WILAYA YA KISII YA KATI
MTIHANI WA MAJARIBIO

DARASA LA 8
Muhula wa pili 2011

KISWAHILI: Sehemu ya Kwanza - Lugha

Muda: Saa 1 Dakika 40

SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala sio katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu.

NAMBA YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO

6. Kwa kujaliza visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mwisho za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
9. Kwa kila swali 1 - 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari kwenye kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndiyo jibu.

Kwa Mfano:

Katika **Kijitabu cha maswali:**

17. Mbwa mdogo sana ni
    A. Kimbwa
    B. Jibwa
    C. Kijibwa
    D. Jimbwa

Jibu sahihi ni C

Katika **Karatasi ya majibu:**

16[A] [B][C] [D] 17[A][B] ~~[C]~~ [D] 18[A][B][C] [D] 19[A] [B][C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya maswali, swali namba 17 kisanduku chenye herufi C ndicho kilichojalizwa.

11. Jaza kisanduku chako vizuri. Kujaliza kwako kuwe kweusi kama inavyowezekana.
12. Kwa kila swali jaliza kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Soma vifungu vifuatavyo. vina nafasi 1-15. Jaza kila pengo kwa kuchagua jibu lifaalo zaidi.

Ukimwi ni _1_ wa kinga mwilini. Wakati huu Ukimwi _2_ tiba, Umesambaa _3_ na unaweza kumfisha mtu _4_. Ukimwi hauna heshima. Kwa wazee, wavulana _5_ mama na wasichana, manasara wala waislamu. _6_ ya ukimwi yanasababishwa na kujuana kimwili na mtu _7_ virusi vyake(VVU). Pia kudungana _8_ pasi _9_ na _10_ damu yenye virusi vya ukimwi.

1. A. Ukosefu B. uhitaji C. upungufu D. uenezaji
2. A. una B. hauna C. hana D. huna
3. A. kote B. kwote C. pale D. wote
4. A. yoyote B. yeyote C. popote D. kokote
5. A. wana B. wa C. na D. akina
6. A. Magonjwa B. Ukongo C. Uwele D. Maradhi
7. A. aliyesambaziwa B. aliyepewa C. aliyeambukizwa D. Aliyepeana
8. A. madawa B. sindano C. dawa D. shindano
9. A. hatari B. tahadhari C. habari D. jabari
10. A. kutiwa B. kuwekewa C. kupimwa D. kutonewa

Kusoma kuna _11_ kubwa. Kunao wanaofikiri kuwa wakishatoka shuleni, hawana hoja ya kusoma. Kuna elimu ya _12_ na elimu ya maisha. Kukamilisha masomo shuleni _13_ mwisho wa elimu _14_ ni mwanzo wa kupata ujuzi, maarifa na hekima inayopatikana vitabuni. Kumbuka elimu ni _15_ .

1. A. dhamani B. thamani C. zamani D. samani
2. A. vitabu B. kitabu C. vitabuni D. shule
3. A. siyo B. sio C. siko D. silo
4. A. ingawa B. mbali C. isipokuwa D. bali
5. A. baharia B. bahari C. hali D. elimu

Kutoka swali la 16-17 jibu swali kulingana na maagizo uliyopewa.

16. Neno 'Tuzo' lapatikana katika ngeli gani?
A. LI-YA B. I-ZI C. I-I D. U- Zi

17. **Andika wingi wa**
Ghulamu alipokonywa hawala na hawara.
A. Maghulamu walipokonywa mahawala na hawara.
B. Ghulamu walipokonywa hawala na mahawara.
C. Maghulamu walipokonywa hawala na mahawara.
D. Maghulamu walipokonywa mahawala na hawara.

18. **"Wanafunzi wanne wa kwanza kufika watatuzwa".**
Kivumishi kilichotumika katika sentensi hii ni cha.
A. Tarakimu B. Idadi C. sifa D. nafsi

19. **Ndugu wa kike na wa kiume huitana _____?**
A. Somo B. umbu C. mnuna D. kaka

20. "Mwambili alimkata karima" Ni kusema kuwa___
A. Alinikatakata nilipokuwa nikilima.
B. Alinisaidia kuruka mlima.
C. Aliyaingilia maongezi yangu kabla sijamaliza kuongea.
D. Aliniendea kichinichini.

21. **Chagua usemi halisi wa:**
Mwalimu aliwauliza iwapo wangeandika insha siku hiyo jioni.
A. "Mtaandika insha kesho jioni?" mwalimu aliwauliza.
B. "kesho jioni mtaandika insha?" mwalimu aliwauliza.
C. "Mtaandika insha leo jioni?" mwalimu aliwauliza
D. "Leo jioni mngeandika insha?" mwalimu aliwauliza.

22. **Ni upi ukubwa na wingi wa:**
Kiti hiki ni cha mzee yule.
A. Makiti haya ni ya majizee yale.
B. Majikiti haya ni ya mazee yale.
C. Majiti haya ni ya mazee yale.
D. Makiti hivi ni vya wazee wale.

23. **Andika kinyume cha sentensi hii.**
Mkemwenza wa yule mfaruku aliuza mbarika wake.
A. Mtanashati wa yule mfaruku aliuza gumba wake
B. Mwanyumba wa yule gumba aliuza beberu wake.
C. Wifi wa yule halati aliuza mori wake.
D. Ajuza wa yule gumba aliuza fahali wake.

24. **Kanusha sentensi ifuatayo**
Baba amekuja na akaandika
A. Baba hajakuja wala kuandika.
B. Baba hajaja wala kuandika.
C. Baba hajakuja na hajaandika.
D. Baba hajaja wala hajaandika.

25. **Tulikula kishuka chetu wakati wa _____.**
A. machwa B. mtikati C. mawio D. majogoo

26. **Akrabu katika uso huu wa saa zinaonyesha saa ngapi?**



A. Saa kumi kasoro dakika kumi
B. Saa nne na dakika kumi
C. Saa kumi na dakika kumi
D. Saa kumi kasoro dakika kumi na tano

27. **Tambua matumizi ya "kwa" katika sentensi**
Wanafunzi walionana na mwalimu wao ana kwa ana.
A. Pamoja na B. matumizi C. sababu D. nahau

28. **Unda kitenzi kutokana na nomino 'MCHESHI'**
A. ucheshi B. cheshi C. cheka D. kicheshi

29. **Ni kiunganishi kipi kilicho sahihi kujazia pengo katika sentensi.**
Sitaki chai _____ uji.

A. sembuse B. licha C. wala D. ingawa

30. Neno "Tia" katika hali ya kutendesha ni:
A. Tosha B. Tiza C. Toza D. Tosa

Soma kifungu kifuatacho. Hatimaye jibu maswali 31-40.

Kwa lugha ya kiingereza, pametokea taifa la Waingereza, na nchi yao ya Uingereza. Waingereza, wawatesa, Waranda na Wasikochi wote walikuwa watu wa mataifa mbalimbali hapo zamani. Hivi sasa wameungana wakawa taifa moja. Nao wakakubali kwamba kiingereza ndiyo lugha ya Uingereza. Aidha kuna mataifa mengine mengi tu ambayo yameungana kuwa taifa moja lenye lugha moja na watu wamoja walio na lugha moja kama vile Ujerumani na Kijerumani, Ujapani na Kijapani, Uchina na kichina, Urusi na Kisusi, ureno na Kireno.

Namna moja ya maarifa ya siasa na utawala haviunganishi watu pamoja. Lugha ndicho chombo kitendacho kazi muhimu katika kuleta mapatano, uelewano na malezi mema ya kweli ulimwenguni.

Bahati njema, Afrika Mashariki tuna lugha ya Kiswahili. Kiswahili kimeweza kuwauunganisha vema watu wetu kuwa taifa moja. Ni bahati mbaya iliyoje kwa baadhi ya watu kufikiri. Kukivunja kiswahili kisisumike ? Hasara kubwa iliyoje kwa warithi wa ukoloni na vizazi vya leo kukosa kuungana. Hawajui kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu?

Lugha ya Kiswahili ina nguvu za kuweza kushindana na upinzani wowote ulimwenguni na kuushinda. Inaweza kuleta maendeleo makubwa zaidi licha ya muungano na uelewano katika Afrika Mashariki na bara la Afrika nzima pia.

Kiswahili ni lugha maarufu na muhimu sana ulimwenguni. Lugha hii hutumika katika nyanja zote za elimu na teknolojia kama vile mitandaoni, tovuti, tarakilishi na mawasiliano ya ulimwengu kwa jumla. Inatangazwa katika idhaa za mataifa makubwa mithili Ujerumani, Uingereza, Uchina, Marekani na kwingineko.

Kiswahili hutumika katika uandishi wa vitabu, majarida, nyaraka na magazeti ya kila siku katika mataifa mengi. Kama huo si ubora na umaanifu, basi udufu uko wapi?

Ama kwa hakika, nchi zetu za Afrika Mashariki tuna udhuru gani wa kuipuuza lugha ya kiswahili hadi kuinyima nafasi ya kukuza uzalendo wetu na kuimarisha umoja tulio nao?

Tuna haki ya kuona fahari kuitumia lugha ya Kiswahili kwa hali na mali. Tutatambua lini kuwa kiswahili ni miongoni mwa lugha kuu za ulimwengu? Wangapi wajuao hivyo kama si Mheshimiwa Rais wa msumbiji, Joakim Chisano na pia mheshimiwa Rais Wa Tanzania, Jakaya Kikwete, ambao wamewahi kuhutubia vikao vya mikutano ya umoja na nchi huru za Afrika kwa lugha ya kiswahili? Vipi mimi na wewe? Tunajivunia kiswahili?

Naam, kama kiingereza ni kwa waingereza wa nchi ya uingereza, sisi na kiswahili chetu hatuwezi kuwa na kiswahili kwa waswahili wa uswahili badala ya kujigawa katika vijitaifa na vijikabila hivi tulivyo navyo? Tunachelea nini? Tunaogopa nini? Lini mpaka lini? Ipo siku.

31. Kauli ipi ni sahihi kulingana na aya ya kwanza, katika taarifa hii.
A. Mataifa mbalimbali yaliungana kuunda taifa kuu la Uingereza.
B. Mataifa mbalimbali yaliungana kuunda taifa kuu la uingereza.
C. Lugha ya Kiingereza iliunganisha taifa la uingereza na mataifa mengine kuwa taifa moja.
D. Lugha ya Uingereza iliwaunganisha Waingereza wakawa taifa moja.

32. Kwa mujibu wa habari uliyoisoma, mwandishi anasema kwamba.
A. Maarifa ya siasa na utawala ni sehemu tu ya muungano wa watu pamoja.
B. Watu wanaweza kuungana vizuri wakiwa na maarifa ya siasa na utawala wa namna moja.
C. Muungano kamili wa mataifa na watu wake huweza kuletwa tu wakiwa na lugha moja.
D. Kila mtu ulimwenguni hupata malezi mema ya kweli akitumia lugha yake.

33. Ni kauli ipi isiyo sahihi kulingana na habari.
A. Hakuna mataifa mengi yaliyounganishwa na lugha yakawa moja ulimwenguni.
B. Ujerumani, Ujapani, Uchina, Urusi na Ureno ni mifano ya uingereza.
C. Uingereza ni mwungano wa mataifa zaidi ya moja.
D. Lugha ya kiingereza ilitumiwa kuyalazimisha mataifa mengi kuungana.

34. Katika Afrika mashariki.
A. Tuna bahati ya kuwa na lugha ya kiswahili inayoweza kutuunganisha.
B. Kiswahili kimepiga hatua kubwa na kuleta mwungano kamili katika nchi zetu.
C. Tunapenda lugha ya kiswahili lakini haiwezi kutuunganisha kamwe.
D. Kiswahili hakitumiki vyema na watu wetu.

35. Ni kina nani miongoni mwa wafuatao wanaokipinga kiswahili kisitumike kikamilifu.
A. Walio na kasumba za kikoloni.
B. Wanaoogopa kusema kiswahili.
C. Watoto au vizazi vya wakoloni.
D. Wanaotaka kurithi ukoloni.

36. Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu ni methali iliyotumika katika taarifa kubainisha kuwa.
A. Watu wakiungana watakuwa na nguvu.
B. Watu wa Afrika mashariki wakitumia kiswahili.
C. Tuna udhaifu mwingi kuliko umoja
D. Hatuna nguvu bila umoja.

37. Lugha ya kiswahili ina nguvu za kuweza kushindana na upinzani gani?
A. Wa mataifa ya nchi
B. Wa wananchi wenye fikra za kikoloni.
C. Wa kutumiwa na mataifa ya nje.
D. Kutoka kwa maadui wa nje ya mataifa yetu na waliomo ndani ya nchi zetu.

38. Umaarufu na umuhimu wa Kiswahili umedhihirika vipi katika ufahamu.
A. Kiswahili hutumika ng'ambo.
B. Kiswahili hutumika katika mawanda yote ya elimu pamoja na mataifa ya ulimwengu.

C. Rais Jakaya Kikwetu na Joakim Chisano walikitumia katika mikutano yao.
D. Afrika mashariki tuna udhuru wa kukipuuza kiswahili.

39. Mwandishi anatubainishia kwamba ipo siku __
A. Kiswahili cha waswahili kitaunda taifa la uswahili.
B. Kiswahili hakina uwezo kuleta umoja wa kwetu ulimwenguni.
C. Ni muhimu kujigawa katika vijitaifa na vijikabila tulivyo hivi sasa.
D. Tumngoje kaka Kuzungu atuletee kiswahili kituunganishe.

40. Anwani ifaayo zaidi kuelcza taarifa hii ni.
A. Kiswahili chetu
B. Lugha ya taifa
C. Matumizi ya kiswahili
D. Ipo siku

Soma kifungu kifuatacho kwa makini kisha ujibu maswali 41-50.

Gusham ameupitisha usiku katika kupiga miayo kwingi na kuhesabu mitambaa panya, dalili wazi kwamba ubao ulikuwa umemshika barabara. Katika hali hii hakuambulia hata lepe moja la usingizi. Kazi yake ya kusomba mizigo ya wasafiri kutoka kwenye vitu vya garimoshi na stani za matwana hadi katikati ya mji sasa imetumbukia nyongo. Kwani ametokea bepari fulani akaimwaga mikokoteni inayoitwa MZEE NI WEWE,zaidi ya elfu sita inayowahundumia wasafiri kila mtaa.

Basi kulipokucha aliona si murua kuendelea kujikalisha mjini na kupakata mikono kama jeta. Aliazimia kuuhama mji arudi zake shambani huku kijijini Morimbocho, maana hakuna faida za mji. Lau kama shauri kuendelea na ukaaji wa mji, basi ingemlazimu na kumjuza kutafuta kibarua kingine. Nacho ni kipi ilhali yeye ni msomi?

Mjini si maskani ya wazembe la sivyo utakuwa kijimelea au kupe mnyonyaji. Nao ukupe haukupi bila kuuma meno, labda uurefushe mkono au akajiuze vichochoroni. Navyo vyote hivyo ni balaa kama si belua. Au tuviite starehe za mbwa kuukalia mkia kama si starehe za paka kunawia mate. Usiwe mtumwa wa njozi. Maisha si lelemama. Hakuna cha msalie mtume wala nabii, kazi ni kujikaza.

41. Ni hali gani iliyomfanya Gusham akapiga miayo na kukosa usingizi?
A. Alipiga moyo konde
B. Alikuwa na njaa
C. Usingizi ulimpata akipiga miayo
D. Hakuna na kazi wala bazi.

42. Giusham alikuwa na dhiki gani moyoni iliyomkera na kumkereketa?
A. Alifirisika
B. Alikosa usingizi usiku kucha
C. Alihesabu mitambaa panya
D. Kibarua kilimwishia akawa hohehohe.

43. Bila shaka, kwa mujibu wa habari hii, Gusham alikuwa _____
A. Mhazili B. Mmachinga C. Hamali D. Mama nitilie

44. Kilicho mvurugia Gusham mchuzi wake wa kufanya kitumbua chake kuingia mchanga ni.
A. Wasafiri walipungua
B. Alifukuzwa kutoka kituoni na kwenye stani.
C. Hakujua kuitumia mikokoteni ya 'mzee ni wewe'
D. Idadi kubwa na mikokoteni iliyompokonya uhamali wake.

45. Kisawe cha' bepari' ni _____.
A. mkulima B. fukara C. maskini D. kabaila

46. Msemo 'kujikalisha na kupakata mikono' ni
A. kukaa mvunguni
B. Kujikakamua
C. Kuzembea au kupiga ubwana
D. Kuwa kupe na kutia mrija.

47. Kauli kuwa "aurefushe mkono" katika habari hii ina maana kuwa.
A. kufanya kazi kwa bidii
B. Kuwa mwizi
C. Kutafuta kibarua kingine
D. Kujiuza vichochoroni

48. Aya ya mwisho inatushauri na kutunasihi kuwa _____
A. Mjini ni makao ya wazembe
B. Starehe za mjini ni za paka na panya.
C. Mtu hakai mjini bila msalie mtume au nabii wake.
D. Maisha ya mjini huhitaji watu wanaotafuta riziki kwa njia halali.

49. Nacho ni <u>kipi</u>, <u>ilhali</u> yeye ni <u>msomi</u> maneno haya yaliyokistariwa ni yapi katika sarufi, ya aina za maneno.
A. Kihuzishi, kiunganishi, kivumishi
B. Kiulizi, kihusishi, nomino
C. Kivumishi, kilinganishi, mtenzi
D. Kiulizi, kiunganishi, nomino.

50. Taarifa hii inatufunza kwamba.
A. Atafutaye hachoki akichoka kesha pata
B. Mtegemea nundu haachi kunona.
C. Mnyonge kupata haki ni mwenye nguvu kupenda.
D. Mchumia juani hulia kivulini.